

»(UDHIBITI WA UGONJWA WA KIDERI) Kuongeza faida ya biashara ya ufgugaji wa kuku kwa kudhibiti kideri«

Ugonjwa wa kideri hauna tiba na ndio muuaji mkubwa wa kuku.

Kuku wenyewe ugonjwa wa kideri wana dalili zifuatazo; kinyesi chao huwa rangi ya kijani na hushikana na manyoya yao, ndani ya mabawa zao kuna mistari ya kijani, kuku hupiga chafya na wanapoachiliwa hukaa katika eneo moja na ni vigumu kutembea kwa sababu ya udhaifu wa miguu. Ikiwa ubongo uamethiriwa, shingo ya kuku inaweza kujipinda na mabawa ya kupooza.

Sababu kideri na udhibiti

Ugonjwa wa kideri husababishwa na vijidudu vidogo vinavyoitwa virusi ambavyo huenezwa na kuku wagonjwa na ndege wengine. Watu ambao wameshika kuku wagonjwa wanaweza pia kueneza ugonjwa. Ni muhimu kutambua kwamba ugonjwa wa kideri unaweza tu kuzuiwa lakini sio kutibiwa.

Ugonjwa wa kideri unaweza kuzuiwa kwa chanjo kwani inasaidia kujenga kingamwili. Kuku waliochanjwa hawaugui iwapo ugonjwa utashambulia. Hata hivyo, chanjo hiyo huchukua muda wa wiki moja kuwa na ufanisi baada ya kutumiwa.

Chanjo za ugonjwa wa kideri

Unapotumia chanjo ya LaSota unapaswa kuhakikisha kwamba kuku wana kiu. Vyombo vyatubaki vya maji vinapaswa kuondolewa usiku kabla ya kuchanja ndege. Kuku hawapaswi kupata maji kwa masaa 2. Ikiwezekana wape chakula kikavu ili kuhakikisha watakuwa na kiu.

Chanjo ya LaSota iliyochanganywa lazima itumike ndani ya saa 2 kwa kuwa ni chanjo ya moja kwa moja. Kwa chanjo ya I-2, kuku hupewa chanjo kwa kuweka tone kwenye jicho moja, na ni bora kutumiwa asubuhi.

Tahadhari

Chanjo zilizosalia zinapaswa kumwagwa kwenye choo cha shimo na kuchomwa, na chupa tupu za chanjo zizikwe. Osha vyombo viliviyotumika wakati wa kuchanja ndege. Chanjo hazipaswi kutumiwa ikiwa zimepita tarehe ya kununuliwa